

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Simu Nambari: 2152532/3  
Baruapepe: [cg@dcea.go.tz](mailto:cg@dcea.go.tz)  
Tovuti: [www.dcea.go.tz](http://www.dcea.go.tz)  
Nukushi: 2152820



8Barabara ya kivukoni,  
S.L.P. 80327,  
Dar es Salaam.

**TAARIFA KWA UMMA**

**KILO 399.28 ZA DAWA ZA KULEVYA ZAKAMATWA**

**Morogoro, 10 Januari, 2023**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imekamata jumla ya kilo 399.28 za dawa za kulevya aina ya bangi katika Kitongoji cha Sokoni, Kijiji cha Chogoali, Kata ya Iyogwe, tarafa ya Gairo, wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro. Ukamataji huo umefanyika kufuatia operesheni iliyofanywa na Mamlaka mkoani humo tarehe 22 Disemba mwaka 2022 ambapo watu wawili wanashikiliwa kuhusika na usafirishaji wa kiasi hicho cha bangi.

Aidha, Watumia hao wamekutwa na bunduki mbili aina ya gobole zenye namba MG-188 na MG-148 pamoja na ngozi ya mnyama anayedhaniwa kuwa ni Kakakuona. Watuhumiwa hao watafikishwa Mahakamani baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inaendelea kufanya operesheni katika maeneo mbalimbali nchini ili kuhakikisha inadhibiti uzalishaji na usafirishaji wa dawa za kulevya.

Imetolewa na,

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Kitengo'.

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**